

JINA

NAMBA YAKO

JINA LA SHULE

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI YA KISWAHILI

2018

Saa 2 ½

(Hati ya kuhitimu elimu ya sekondari Kenya (K.C.S.E)

MAAGIZO

- Jibu maswali manne pekee
- Swali la kwanza ni la lazima;
- Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani tamthilia ,hadithi fupi, fasihi simulizi na ushairi.

Karatasi hii ina kurasa 4. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote zmepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

Swali la kwanza la (lazima)

RIWAYA

Z. BURHANI: Mwisho wa kosa

1. “Undugu ni kufaana, sio kufanana .” Jadili ukweli wa kauli hii kwa mujibu wa riwaya ya mwisho wa kosa (alama 20)

TAMTHILIA

KITHAKA WA MBERIA : Kifo kisimani

Jibu swali la 2 au la 3

2. “Ujeuri , mwenzangu ni kidonda . Kitilie dawa”
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
 - b) Kando na mzungumziwa, taja na ueleze wahusika wengine waliotawaliwa na ujeuri na jinsi ulivyowaathiri (alama 6)
 - c) Eleza mbinu ya uandishi iliyotumiwa kwenye dondoo hili (alama 2)
 - d) Eleza usawiri wa mwanamke katika tamthilia ya kifo kisimani (alama 8)
3. Huku ukitoa mifano maridhawa, jadili dhana kuwa tamthilia ya kifo kisimani inamulika na kipiga vita utawala dhalimu katika mataifa ya kiafrika (alama 20)

HADITHI FUPI

K.W WAMITILA : Mayai waziri wa maradhi

Jibu swali la 4 au la 5

4. Ukirejelea Hadithi ya ‘ Mkimbizi’ angazia madhara ya ukimbizi na mapendekezo ya utatuzi (alama 20)
5. Hadithi ‘ uteuzi wa moyoni’ na ‘ Ngome ya nafsi ‘ zimedhihirisha taasubi ya kiume na utamaduni unaomkandamiza mwanamke. Thibitisha (alama 20)

FASIHI SIMULIZI

- 6 a) Maghani ni nini? (alama 2)
- b) Eleza fani zifuatazo za maghani
 - i) Vivugo
 - ii) Tondozi
 - iii) Pembezi
 - iv) Rara (alama 8)
 - b) Eleza maana ya neno **ULUMBI** (alama 2)
 - c) Bainisha sifa tisa (a) za mlumbi (alama 8)

USHAIRI.

Soma shairi lifuatali na ujibu maswali yake.

Ziumiazo N'Nyasi

1. Yawile matononofu majani hali yoyote iwavyo
Yefura ukamilifu majani yalikiota viliyvo
Pamoja yali makifu majani kwa jinsi mambo yendayo
Fahali kayatilifu majani ndivyo igeuke sivyo
Wanapowana fahali ziumiazo n' nyasi
2. Ingawa yali dhaifu majani pamoja yalishikana
Ama katika wakifu majani au kwa kusadiana
Ndugu yali bainifu majani tokea zamani sana
Yakapondwa bila hofu majani fahali walipowana
Wanapowana fahali ziumiazo n' nyasi
3. Pondaponda mepondeka majani fahali waktivutana
Tena yakatawanyika majani kwa jambo lisilo kina
Yakabaki kudhiika majani ndugu wanaofanana
Fahali wanayacheka majani wala habari hawana .
wanapowana fahali ziumiazo n' nyasi
4. Fahali wanapotaka yakini hata hutembeleana
Na makoo kadhalika yakini wanapotaka kuonana
Ndama pia watawuka yakini ng'ambu ile kulishana
Tena nyasi hazeshika yakini karibu hazikutana
Wanapowana fahali ziumazo n'nyasi.
5. Si ndaamba si ukoka majani si mbuga si wanda tena
Yamebaki mabaka majani vipande kuoteana
Kwa machaka hayeshika majani hayawezi kupachana
Na fahali watimka majani 'ngali wakisuguana
Wanapowana fahali ziumiazo n' nyasi

MASWALI:

- a) Mwandishi ana ujumbe gani katika shairi hili? (Alama 2)
- b) Eleza muundo wa shairi hili (Alama 3)
- c) Mwandishi amefauluje katika kutumia uhuru wa kishairi? (Alama 3)
- d) Huku ukitoa mifano eleza mbinu za uandishi alizotumia mwandishi? (Alama 2)
- e) Andika ubeti wa pili katika lugha nathari (Alama 5)
- f) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi (Alama 3)
- i) matononofu
- ii) mabaka
- iii) kupachana
- g) Taja bahari za shairi hili q (alama 2)